We've updated our Privacy and Cookies Policy

We've made some important changes to our Privacy and Cookies Policy and we want you to know what this means for you and your data.

OK

Find out what's changed

# Mzozo Khartoum unaacha wapi mustakabali wa amani Sudan kusini?

18 Aprili 2019



AKUOT CHOL

**Rais Salva Kiir wa Sudan kusini amejitolea kuwa mpatanishi katika kuidhinisha mageuzi ya kisiasa nchini Sudan baada ya kupinduliwa kwa kiongozi aliyekuwepo Omar al-Bashir, Reuters linaripoti.**

Hatua hii inajiri miezi saba baada ya Bashir kusaidia katika upatanishi na kufikiwa makubaliano ya amani kati ya Rais Kiir na kundi kuu la waasi wa upinzani Sudan kusini , uliosaidia kupata uhuru wa taifa hilo changa barani Afrika baada ya mapigano ya miongo kadhaa.

"Rais amejitolea kuwa mpatanishi katika majadiliano ya makundi tofauti nchini Sudan kwa matumaini kwamba mageuzi mapya yataidhinisha siku mpya Sudan...," Reuters limenukuu taarifa ya ofisi ya rais.

- **Korea Kaskazini yadai kufanyia majaribio 'silaha mpya'**
- **HIV yatumika kuwaponya watoto**
- **Tuzo ya BBC ya Mwanakandanda bora wa kike 2019**

Mzozo wa kisiasa na wa kiaraia nchini Sudan umegubika majadaliano, lakini hali inayojiri nchini humo inatazamwa vipi kutoka Sudan Kusini?

Swali kubwa ni vipi taifa hilo litakavyofanikiwa katika pendekezo hili sasa?

Inafahamika kwamba Bashir alikuwa na jukumu kubwa katika kufikiwa makubaliano ya amani Sudan Kusini.

ASHRAF SHAZLY

## Historia ya Sudan mbili

Mataifa hayo mawili yana historia ndefu na huenda ndio sababu Sudan Kusini inaona ina wajibu wa kuhusika katika yanayoshuhudiwa hivi sasa Sudan.

Sudan kusini ilijitenga na Sudan mnamo 2011 na miaka miwili baada ya hatua hiyo kubwa, taifa hilo changa lilitumbukia katika vita vya kiraia.

Takriban watu 400,000 wameuawa na karibu thuluthi ya idadi jumla nchini imeachwa bila ya makaazi.

**Rais Salva Kiir** na aliyekuwa makamu wake Riek Machar wametia saini **makubaliano ya amani** hivi karibuni kumaliza mzozo huo wa miaka mitano.

Ni makubaliano yaliofikiwa kwa usaidizi wa Sudan, lakini jana Riek Machar alisema hayuko tayari kurudi Juba na anataka mipango ya kuunda serikali ya muungano iahirishwe mpaka masuala ya usalama yatakapo tatuliwa nchini.

- **Je mapinduzi ya kijeshi yanaongezeka Afrika?**
- **Wasifu wa Omar al-Bashir Sudan**

Siku chache zilizopita rais Salva Kiir pia amesema haoni uwezekano wa kuundwa serikali ya muungano mwezi ujayo na kuongeza kwamba masuala ya usalama hayajatatuliwa.

Wanaharakati mjini Juba wana wasi wasi mwingi kuhusu uwezekano wa kufikia makubaliano katika mzozo ambao kiini chake ni masuala ya usalama.

'Wasiwasi wa usalama utabaini amani ya kudumu Sudan kusini na tunavyozungumza muungano wa vikosi haujaidhinishwa na mpango huo bado upo katika kiwango cha awali na muda umesogea, kwahivyo hili linawatia wasiwasi wengi' anasema Sarah Nyanath, afisa katika jukwa la mashirika ya kiraia Sudan kusini.

ASHRAF SHAZLY

## Hali Khartoum inaacha wapi mustakabali wa amani Sudan kusini?

Akizungumzana BBC Bi Nyanath ameeleza kwamba hali nchini Sudan ina athari kubwa kwa mustakabali wa amani Sudan kusini.

'Ilituchukua miezi mingi katika majadiliano huko mjini Addis Ababa Ethiopia, na kilichochangia kujivuta kwa mazungumzo hayo ilikuwa ni suala la usalama. Lakini wakati mazungumzo yalipohamishwa Sudan, Na kutokana na uzoefu na uelewa wa Bashir kuhusu taifa la Sudan kusini, alisaidia sana kusukuma mazungumzo hayo na kufika mahali tulipofika.

Na sasa vile kunashuhudiwa mabadiliko katika utawala wa Khartoum, hatujui ni nani anayeingia kushikilia usukani'.

Nyanath anasema raia Sudan kusini wana wasiwasi zaidi kutokana na kwamba waandamanaji Khartoum wanaonekana hawana ajenda ya pamoja.

'Kwa kuangalia sababu ya kufanyika maandamano hayo ambayo awali yalikuwa ni ya kulalamikia gharama kubwa ya maisha, yakawa ya kushinikiza mageuzi ya utawala na sasa mambo mengine yanaibuka katikati ya maandamano hayo, ikiwemo baadhi wanaoshinikiza muungano wa Sudan itakayojumuisha Sudan yetu (ya kusini) ambayo tayari imejitangazia uhuru'.

'Ina tia wasiwasi, wakati waandamanaji wanaendelea kushinikiza huenda idara mbali mbali zikagawanyika au zikakataa kusikiza matakwa ya raia, na haya ni wakati tuna idadi kubwa ya wakimbizi nchini humo, na zaidi ya hayo Khartoum ikiwa ni mdhamini mkuu katika makubaliano ya amani, ikiwemo jitihada za kuundwa serikali ya muungano ambayo kufikia sasa hata haijaundwa' anaeleza Bi Nyanath.

STEFANIE GLINSKI

Ameongeza kwamba haya yote yanachangia wasiwasi na maswali mengi kuhojiwa kwa sasa.

Inaarifiwa kwamba serikali ya Sudan kusini imetuma ujumbe mjini, Khartoum, kwa miongini mwa mengine, kuahidi kuwajibikia uhusiano kati ya mataifa hayo mawili.

"Mheshimiwa rais amehakikisha kuunga mkono mageuzi ya amani yatakayo idhinisha siku mpya Sudan ambako amani, umoja na heshima ya mipaka na uhuru wa watu wa Sudan utahakikishwa." **Linaripoti gazeti la South Sudan News Now kwa kunukuu ujumbe wa kutoka ikulu ya rais.**

Raia Khartoum wanasema watasalia katika maandamano mitaani mpaka wakati ambapo viongozi wa kijeshi ambao wanashikilia madaraka hivi sasa, watakabidhi uongozi wa nchi kwa utawala wa kiraia.


## Mada zinazohusiana

**Maandamano** **Sudan** **Siasa** **Maandamano** **Afrika** **Sudan Kusini**

## Mshirikishe mwenzako Unavyoweza kumshirikisha mwenzako

Rejea mwanzo wa ukurasa

## Maelezo zaidi kuhusu taarifa hii

**Utawala wa miaka 30 wa Omar al-Bashir Sudan**
11 Aprili 2019

**Sudan: Je mapinduzi ya kijeshi yanaongezeka Afrika?**

12 Aprili 2019

**Mapinduzi ya jeshi Sudan: Omar al-Bashir aswekwa jela baada ya kupinduliwa Sudan**

17 Aprili 2019

**Mzozo Sudan: Baraza la kijeshi lawakamata waliokuwa maafisa wa serikali**

15 Aprili 2019

## Habari kuu

**Rais wa Burundi Pierre Nkurunziza aaga dunia**
Rais wa Burundi Pierre Nkurunziza aaga dunia
9 Juni 2020

**Matukio ya 'wasiojulikana' Tanzania**
9 Juni 2020

**Kiongozi wa upinzani Tanzania avamiwa na kushambuliwa**
9 Juni 2020

## Gumzo mitandaoni



**Kwanini niliamua kutoitazama video ya mauaji ya George Floyd**




**Corona imewalazimisha kuendeleza fungate isiyoisha**

**Kijiji cha Afrika Kusini kilichopo katika hatari ya corona**

**Mwanamichezo, rafiki na baba - George Floyd alikuwa nani?**

**Simba wamshambulia na kumjeruhi mwanamke Australia**

**Auawa kwa 'kufunga ndoa' kisiri Iran**

**Ndege huyu alisafiri vipi umbali mrefu zaidi?**

## Habari zilizosomwa zaidi

Rais wa Burundi Pierre Nkurunziza amepatwa na mshtuko wa moyo akiwa na miaka 55 **1**

Tanzania: Kiongozi wa upinzani Freeman Mbowe avamiwa na kushambuliwa **2**

Tatizo la Android: Kwa nini picha hii ni hatari kwa simu yako? **3**

Matukio ya 'wasiojulikana' yaliyoibua gumzo nchini Tanzania **4**

Tetesi za Soka Ulaya Jumanne 09.06.2020: Fati, Van de Beek, Gerson, Ngakia, Mkhitaryan 5

## Uongozaji BBC

News

Weather

Arts

Sport

Radio

Masharti ya matumizi

Sera ya Faragha

Accessibility Help

Wasiliana na BBC

Jitangaze na BBC

Kuhusu BBC

Cookies

Parental Guidance

Get Personalised Newsletters

Chaguo

**Copyright © 2020 BBC.** BBC Haiwajibiki kwa taarifa kutoka tovuti zisizo zake. **Muongozo wetu kuhusu na juu ya wavuti za nje.**